


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S. L.P 1055, ARUSHA  
Simu : (027) 2503538/ 2507928  
Nukushi: (027) 2505973  
Barua pepe: [rbcarusha@pccb.go.tz](mailto:rbcarusha@pccb.go.tz)  
Wavuti : [www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**JUNI 26, 2020**

**MAJI YA KIJIKI YAMPONZA MWENYEKITI WA KITONGOJI**

TAKUKURU Mkoani Arusha, mnamo Juni 25, 2020 ilimkamata Daniel Luka Mollel ambaye ni Mwenyekiti wa Kitongoji cha Olmotony kilichopo Kata ya Olmotony, Mji Mdogo wa Ngaramtoni, katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, kwa kupokea rushwa ya kiasi cha shilingi elfu sabini (sh. 70,000/-) kutoka kwa Nai Joseph mkazi wa kitongoji cha Olmotony ili aweze kumuunganisha katika mtandao wa maji ya kijiji.

Mtuhumiwa huyo anatarajiwa kufikishwa mahakamani leo tarehe 26.06.2020 kwa kosa la kuomba na kupokea rushwa ambalo ni kinyume na kifungu cha 15 (1) (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

**Ufafanuzi wa Makosa:**

TAKUKURU mkoa wa Arusha, ilipokea taarifa mnamo tarehe 25.06.2020 kutoka kwa **Nai Joseph** mkazi wa kitongoji cha Olmotony, akieleza kwamba katika kitongoji chao kuna mtandao wa maji ambao huunganishwa BURE kwa wananchi baada ya kukamilisha taratibu za kuchukua fomu ofisi ya kitongoji, kuijaza na kuirudisha.

Ilielezwa pia kwamba hata baada ya mwananchi kuunganishiwa maji hayo, hakuna gharama yoyote anayolipa mhusika aliyeunganishiwa maji.

Mlalamikaji alieleza kwamba pamoja na kufahamika kuwa maji hayo husambazwa bure kwa wananchi, Mwenyekiti wa Kitongoji **Daniel Luka Mollel** amekuwa akiwatoza wananchi wanaofika ofisini kwake kutaka kuunganishiwa maji, kiasi tofauti tofauti cha fedha ili waweze kupata maji hayo.

Nai anaendelea kueleza kwamba, mnamo Juni 21, 2020, alifika ofisi ya kitongoji kwa ajili ya kupata mwongozo wa namna ya kupata huduma ya maji na kwamba alionana na mwenyekiti huyo wa kitongoji ambaye alimweleza kuwa, ili aweze kuunganishiwa maji anapaswa kuandika barua ya maombi na kuiwasilisha ofisini kwake ila aambatanishe na "CHAI" kwa maana ya fedha.

Nai anaeleza kwamba aliandika barua hiyo na kuipeleka ofisini kwa mwenyekiti wa kitongoji lakini hakumkuta na kwamba aliporudi nyumbani alikuta mume wake ambaye alikuwa safarini amewasiliana na vijana wanaohusika kuunganisha maji, nao wakaja wakaunganisha maji.

Alieleza kwamba baada ya mwenyekiti kufahamu kuwa ameunganishiwa maji, alifika nyumbani kwake na kuanza kumgombeza mlalamikaji kwa kuunganisha maji bila kufuata utaratibu. Baadaye Mwenyekiti huyo alimweleza kuwa iwapo anataka jambo hilo liishe,apeleke barua ya maombi ya maji ofisini kwake akiwa ameambatanisha fedha kiasi cha shilingi laki moja (sh. 100,000/-).

Baada ya kupokea taarifa hiyo na kufanya uchunguzi wa awali, TAKUKURU mkoa wa Arusha iliandaa mtego wa rushwa ambapo fedha kiasi cha sh. 70,000/- kiliambatanishwa na barua ya maombi na kupelekewa mwenyekiti huyo wa kitongoji. Mwenyekiti huyo alipokea fedha hizo na kuahidi kutomsumbua tena mlalamikaji Nai.

TAKUKURU Mkoa wa Arusha inawashukuru wananchi kwa kuiamini TAKUKURU na kuendelea kuipa ushirikiano kwa kutoa taarifa za wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwenye taasisi za Serikali na maeneo mengine. Hii inaashiria mwamko chanya wa wananchi katika kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa.

TAKUKURU mkoa wa Arusha inawahamasisha wananchi kuendelea kutoa taarifa hasa katika kipindi hiki tunachoelekea kwenye maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na kuwahakikishia kuwa taarifa zitakazopokelewa zitafanyiwa kazi kwa haraka na hatimaye kuwezesha kupatikana kwa viongozi wasiotoa rushwa ili kuchaguliwa.

Aidha TAKUKURU Mkoa wa Arusha inatumia fursa hii kuwaonya wale wote walioanza kuwarubuni wapiga kura kwa rushwa na kufanya kampeni kabla ya, wakati, kwamba vitendo hivyo wanavyovifanya ni kinyume cha sheria na wakibainika watachukuliwa hatua kali.

**Imetolewa na:**

**JAMES G. RUGE**

.....

**KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) ARUSHA**

.....